



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

**WAJIBU WA VYAMA VYA SIASA NA WAGOMBEA WAKATI WA
KAMPENI, UTEUZI WA MAWAKALA WA VYAMA VYA SIASA NA
UTANGAZAJI WA MATOKEO**

Tarehe 20 Oktoba, 2020

Zikiwa zimebaki siku 8 kufikia tarehe 28 Oktoba, 2020 ambayo ndio siku ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatumia nafasi hii kuvikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wananchi kwa ujumla kuwa Ibara ya 26 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaweka masharti kuwa, kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii Katiba na sheria za Jamhuri ya Muungano.

Kama tunavyofahamu kampeni za uchaguzi zinaendelea katika maeneo mbalimbali kwa vyama vya siasa na wagombea wa ngazi zote. Tume inatumia nafasi hii kuvipongeza vyama na wagombea ambao wanandelea na kampeni kwa mujibu wa Sheria, kanuni na maadili ya uchaguzi.

Eneo la pili ambalo ni muhimu kukumbushana ni hili la **mawakala wa vyama vya siasa**. Tume inavikumbusha vyama vya siasa kuwa kesho tarehe 21 Oktoba, 2020 vinatakiwa kuwasilisha orodha na barua za utambulisho wa mawakala wa vyama vyao kwa wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo husika. Utaratibu wa kuteua mawakala, kuwaapisha, kuwapangia vituo na utambulisho wao kwa wasimamizi wa vituo umeanishwa chini ya kifungu cha 57 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, na kifungu cha 58 cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, vikisomwa pamoja na kanuni za 50 na 43 zilizotungwa chini ya sheria hizo.

Aidha, utaratibu huu wa kisheria umefafanuliwa katika vijitabu vya Maelekezo kwa Vyama vya Siasa na Wagombea na Maelekezo kwa Mawakala wa Vyama vya Siasa na Wagombea vya mwaka 2020 ambavyo tayari Tume imevipatia vyama vya siasa. Vivyo hivyo, ufafanuzi huu umetolewa kwa kina kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Jambo la tatu na muhimu kukumbushana ni kuhusu **mamlaka za kutangaza matokeo ya uchaguzi** wa Rais, Wabunge na Madiwani. Chini ya Ibara ya 41(7) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 81 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na Kifungu cha 82 cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais, Wabunge

na Madiwani yametolewa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi.

Kwa msingi huu, kikundi, taasisi, chama cha siasa au mtu yoyote atakayetangaza matokeo ya uchaguzi ya ngazi yoyote, kabla ya mamlaka rasmi zilizowekwa kikatiba na kisheria kufanya hivyo, atakuwa amevunja sheria na hatua stahiki za kisheria zitapaswa kuchukuliwa dhidi yake.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi haitarajii kuona kikundi, taasisi, chama cha siasa, wagombea na wafuasi wao au mtu yoyote akijichukulia sheria mikononi ya kutangaza matokeo ya uchaguzi nje ya utaratibu na mamlaka zilizowekwa kikatiba na kisheria.

Jaji Rufaa (Mst.) Semistocles Kaijage

MWENYEKITI

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI